

TANGAZO LA SERIKALI NA. 341 la tarehe 3/5/2024

**SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,  
(SURA YA 272)**

**NOTISI**

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 9(1) na (2))*

NOTISI YA KUONGEZA ENEO LA KUTOA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA  
MAZINGIRA, MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA BABATI YA MWAKA  
2024

Jina 1. Notisi hii itajulikama kama Notisi ya  
Kuongeza Eneo la Kutoa Huduma za Maji na Usafi wa  
Mazingira, Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira  
Babati ya Mwaka 2024.

Kuongezwa 2. Eneo la huduma la Mamlaka ya Maji na Usafi  
eneo la huduma wa Mazingira Babati linaongezwa kujumuisha maeneo  
yaliyoainishwa katika Jedwali.

Kufutwa 3.-(1) Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira  
kwa Mamlaka ya Orkesumet inafutwa.  
Maji

(2) Haki, wajibu, masharti ya ajira ya watumishi,  
mali, madeni na masuala mengine yanayohusika  
yaliyotolewa au yaliyokuwa yakitekelezwa na Mamlaka  
ya Maji na Usafi wa Mazingira iliyofutwa  
yanakabidhiwa kwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa  
Mazingira Babati.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

JINA LA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA	ENEO LA LINALOONGEZA	HUDUMA
--	-------------------------	--------

*Notisi ya Kuongeza Eneo la Kutoa Huduma za Maji Na Usafi wa Mazingira,  
Mamlaka ya Maji Na Usafi wa Mazingira Babati*

*Tangazo La Serikali Na. 341 (Linaendelea)*

Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Babati.	Wilaya ya Simanjiro kwenye Kata tano zifuatazo: 1. Orkesumet; 2. Langai; 3. Edonyongijape; 4. Ruvu Remit; na 5. Lobosit.
---	---

Dodoma,  
7 Aprili, 2024

JUMAA HAMIDU AWESO  
*Waziri wa Maji*